

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

Tele: +255 0262322761-5

Fax No. +2550262324218

Email: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge

S.L.P 941

DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 10 Novemba, 2017, Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam ilitoa uamuzi wa awali katika shauri (*Misc Civil Application No: 479 of 2017*) lililofunguliwa na waliokuwa Wabunge nane (8) wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Viti Maalum kupitia Chama Cha Wananchi (CUF).

Uamuzi huo wa mahakama ni wa awali uliotolewa kwenye mapingamizi ya awali na uliwalenga walalamikiwa ambao ni Baraza la Wadhamini wa CUF pamoja na uongozi wake ambao uliamuru kuwa walalamikiwa wasitisha utekelezaji wa uamuzi wa kuwafukuza uanachama (*suspension of the implementation of the expulsion order*) na vilevile, kutojadili suala lolote kuhusu uanachama wa Walalamikaji hao hadi Mahakama itakapokamilisha kusikiliza shauri la msingi. Shauri hilo lilifunguliwa kupinga uamuzi wa CUF kuwafukuza uanachama na kwa mujibu wa kumbukumbu za Mahakama bado uamuzi wa mwisho kuhusu shauri hilo haujatolewa.

Ni vema ifahamike kuwa, hakuna sehemu yeyote katika uamuzi huo wa Mahakama **inapoeleza kuwa Wabunge hao wanatakiwa kurudishiwa ubunge wao.**

Kumekuwepo tafsiri isiyo sahihi ya uamuzi huo wa Mahakama inayotolewa na baadhi ya watu na vyombo vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii kusambaza taarifa potofu kwamba Wabunge waliofukuzwa na CUF wamerejeshwa Bungeni kwa uamuzi wa Mahakama baada ya kurejeshwa uanachama wa CUF. Waliokuwa Wabunge pia wameiandikia Ofisi ya Bunge wakiomba kufahamishwa utaratibu utakaotumika kuwarejesha Bungeni.

Tunapenda umma uelewe kwamba, nafasi za Ubunge zilizoachwa wazi baada Wabunge husika kufukuzwa uanachama, zilijazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria, na Wabunge waliopatikana kujaza nafasi hizo wanaendelea kutekeleza majukumu yao ya kibunge ipasavyo.

Imetolewa na;

KATIBU WA BUNGE

30 Novemba, 2017